**MAELEZO YA MWENYEKITI WA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**MHESHIMIWA JAJI (RUFAA) JACOBS C. M. MWAMBEGELE**

**KATIKA UZINDUZI WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA MKOANI KIGOMA**

**TAREHE 20 JULAI, 2024**

- **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**
- **Mheshimiwa Ummy Nderiananga (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu),**
- **Mheshimiwa Zainab Katimba (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,**
- **Mheshimiwa Jaji George Joseph Kazi, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar,**
- **Mheshimiwa Jaji wa Rufaa (Mst.) Mbarouk Salim Mbarouk, Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi,**
- **Waheshimiwa Wajumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi,**
- **Ndugu Ramadhani Kailima, Mkurugenzi wa Uchaguzi - Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi,**

- **Mheshimiwa Kamishna Generali wa Zimamoto na Uokoaji (Mstaafu) Thobias Andengenye – Mkuu wa Mkoa wa Kigoma,**
- **Mheshimiwa Nyangindu Boniphace Butondo – Mbunge wa Kishapu – kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Katiba Sheria na Utawala,**
- **Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa mliopo,**
- **Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**
- **Waheshimiwa Mabalozi Wanaowakilisha Nchi Mbalimbali,**
- **Waheshimiwa Wabunge,**
- **Viongozi wa Dini,**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Wageni Waalikwa na Ndugu Wananchi,**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

*Mheshimiwa Waziri Mkuu,*

Awali ya yote na kwa niaba ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha hapa katika uwanja wa Kawawa mkoani Kigoma leo tarehe 20 Julai, 2024 kwa ajili ya shughuli ya uzinduzi rasmi wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Pili, kipekee kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kukubali wito wetu na kutenga muda wako ili kuwa mgeni rasmi katika siku hii muhimu. **TUNAKUSHUKURU SANA.**

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Kwa mujibu wa ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 10(1)(a) na(b) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya mwaka 2024, Tume imepewa majukumu kadhaa ikiwemo kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani kwa Tanzania Bara.

Aidha, masharti ya kifungu cha 16(5) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024, Tume ina wajibu wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili kati ya kipindi kinachoanza baada ya uchaguzi mkuu mmoja na kabla ya siku ya uteuzi wa uchaguzi mkuu unaofuata.

Mara ya mwisho Tume kuboresha Daftari ilikuwa mwaka 2019/2020. Hivyo, uzinduzi utakaoufanya ni uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa awamu ya kwanza unaoanza leo tarehe 20 Julai, 2024 na kukamilika Machi, 2025 ili kutoa nafasi kwa uboreshaji wa awamu ya pili.

*Mheshimiwa Waziri Mkuu,*

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utafanyika katika mizunguko (routes) 13 na leo ndiyo unaanza mzunguko wa kwanza utakaohusisha mikoa mitatu ya Kigoma, Tabora na Katavi. Zoezi la uboreshaji kwa kila mzunguko (route) litadumu kwa muda wa siku saba ambapo vituo vya kuandikisha vitafunguliwa saa mbili kamili (2:00) asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili kamili (12:00) jioni ya kila siku kwa kila kituo.

*Mheshimiwa Waziri Mkuu,*

Kwa upande wa Zanzibar, kama inavyoonekana kwenye ratiba ya uboreshaji, zoezi hili litafanyika kuanzia tarehe 07 hadi 13 Oktoba, 2024, na kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13 (1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024 uboreshaji wa Daftari utamhusu mtu yeyote aliyepo Zanzibar ambaye hana sifa za kuandikishwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) lakini anayo sifa ya kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano.

*Mheshimiwa Waziri Mkuu,*

Jumla ya **vituo 40,126** vitatumika katika zoezi la uboreshaji wa Daftari. Kati ya hivyo, **vituo 39,709** vipo Tanzania Bara na **vituo 417** vipo Tanzania Zanzibar.

Idadi hii ya vituo ni ongezeko la **vituo 2,312** zaidi ikilinganishwa na **vituo 37,814** vilivyotumika kuandikisha Wapiga Kura kwa mwaka 2019/2020.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Kwa mujibu wa Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2022, tunatarajia kuandikisha wapiga kura wapya **5,586,433** ambao wametimiza umri wa miaka **18** na ambao watatimiza umri huo kabla au ifikapo siku ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Sanjari na hao tunatarajia wapiga kura **4,369,531** wataboresha taarifa zao na wapiga kura **594,494** wataondolewa kwenye Daftari kutokana na kukosa sifa za kuendelea kuwemo kwenye Daftari kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo vifo, kukana uraia au kupoteza sifa za kuendelea kuwemo kwenye Daftari.

Aidha, kwa kuzingatia kifungu cha 10 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024, uboreshaji wa mwaka huu utahusisha wafungwa / wanafunzi wanaotumikia kifungo cha chini ya miezi sita na mahabusu waliopo kwenye magereza Tanzania Bara na Vyuo vya Mafunzo Tanzania Zanzibar.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Tume imehuisha mifumo ya uandikishaji wa wapiga kura na kwa uboreshaji unaoanza leo, wananchi waliopo kwenye Daftari wanaweza kuanzisha

mchakato wa kuboresha taarifa au kuhamisha taarifa zao wakiwa nje ya kituo cha kuandikisha wapiga kura kwa njia ya kielekroniki kwa kutumia simu ya mkononi au kompyuta na kisha kufika kituo cha kuandikisha wapiga kura kukamilisha mchakato wa kuweka saini, kupigwa picha na kupewa kadi yake ya mpiga kura.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Tume imefanyia kazi maoni ya wadau mbalimbali, walioomba mfumo wa kuanzisha mchakato wa kuboresha au kuhamisha taarifa kwa njia ya simu, pia uwezeshe wenye simu za kawaida (maarufu kwa majina ya kitochi au kiswaswadu) kuanzisha mchakato huo.

Napenda kuchukua nafasi hii kutoa taarifa rasmi kwamba, kuanzia leo tarehe 20 Julai, 2024 pamoja na huduma hiyo kupatikana kwenye simu janja lakini pia wale wenye simu za kawaida (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) watapata huduma hiyo kwa kupiga **USSD Code *152*00# na kubonyeza namba 9** kisha kuendelea na hatua zingine kama itakavyokuwa inaelekezwa kwenye simu husika.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Maandalizi yote muhimu kuhusiana na uboreshaji yamekamilika ikiwa ni pamoja na ununuzi wa BVR Kits 6,000. BVR hizi zinatumia mfumo wa

programu endeshi ya *android* na zina uzito wa kilo 18, tofauti na BVR Kits zilizotumika mwaka 2015 na 2020 zenye uzito wa kilo 35 na programu endeshi ya *window.* Vifaa vingine muhimu vilivyonunuliwa ni pamoja na kadi mpya, wino na makasha ya kubebea vifaa na fomu mbalimbali za uboreshaji.

Aidha, Tume imeshaandaa na kuchapisha kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za mwaka 2024, maelekezo na miongozo mbalimbali inayohusiana na zoezi hili.

Kama sehemu ya maandalizi, Tume imefanya uteuzi wa watendaji mbalimbali wa uboreshaji. Watendaji hao ni Waratibu wa Uandikishaji wa Mikoa, kwa mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, Maafisa Waandikishaji wa Jimbo 184, Maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Jimbo 792, Maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Kata 3,956, Maafisa TEHAMA 368, Maafisa Ugavi wa Halmashauri au Maafisa Manunuzi 184 na Maafisa Uchaguzi 184, kwa halmashauri zote za Tanzania Bara.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Hadi kufikia tarehe ya leo, Tume imeshakutana na wadau muhimu wa uchaguzi kwenye mikutano mbalimbali iliyoanza tarehe 07 Juni, 2024.

Miongoni mwa wadau tuliokutana nao katika ngazi ya Taifa ni vyama vya siasa 19 vyenye usajili kamili, wawakilishi wa wanawake, vijana, watu wenye ulemavu, wahariri wa vyombo vya habari, waandishi wa habari na maafisa

habari kutoka katika halmashauri zote za Tanzania Bara. Mikutano ya aina hii imefanyika pia katika mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora na itaendelea kufanyika katika mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzingatia ratiba ya mzunguko wa uboreshaji (routes).

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Mbali ya mikutano ya wadau kufanyika, Tume imewapatia wadau wote ratiba ya uboreshaji wa Daftari, Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024, Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya mwaka 2024, miongozo na maelezo kuhusu uboreshaji.

Aidha, vyama vya siasa vilipatiwa orodha ya vituo vya kuandikisha wapiga kura na vitapewa fursa ya kuweka mawakala wa uandikishaji katika vituo vyote vitakavyotumika kuandikisha wapiga kura.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Tume imeendelea kutoa elimu ya mpiga kura na itaendelea kutoa elimu hiyo wakati wote wa kipindi cha uboreshaji. Elimu inatolewa kupitia vipindi vya Televisheni, Redio, Makala kwenye magazeti na majarida, mitandao ya kijamii ya Tume, Tovuti, Televisheni na Redio mtandao za Tume pamoja na vipindi vya mijadala inayoendeshwa na Tume au inapoalikwa na wadau mbalimbali ili kuwapa uelewa kuhusu uboreshaji.

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 10(1)(h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya mwaka 2024, Tume imetoa vibali kwa taasisi na asasi **157** zitakazotoa elimu ya mpiga kura katika kipindi chote cha uboreshaji.

Aidha, kwa kuzingatia dhana ya uwazi katika zoezi hili pamoja na masharti ya kanuni ya 46 (1) (4) ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Mwaka 2024, Tume imetoa vibali kwa taasisi na asasi **33** za ndani na **8** za kimataifa kuwa Waangalizi wa Uandikishaji kwa ajili ya kutazama uendeshaji wa zoezi la uboreshaji.

Taasisi na asasi zote zilizopewa kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura na uangalizi wakati wa zoezi la uboreshaji, zimepewa nyaraka mbalimbali ikiwemo Katiba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, Sheria na miongozo inayosimamia jukumu la utoaji wa elimu ya mpiga kura na utazamaji katika zoezi hili.

Tume itaendelea na wajibu wake kuhakikisha taasisi za asasi hizo zinatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria na kanuni.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Katika kuboresha huduma kwa wapiga kura wetu, tumefungua kituo cha huduma kwa mpiga kura (call centre) kwa ajili ya kuwawezesha wapiga kura au wanaotarajiwa kuandikishwa au kuboresha taarifa zao na kupatiwa

ufafanuzi, majibu au maelezo ya maswali au hoja zinazohusu zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Huduma hii ambayo ni bure imeanza kutumika tarehe 18 Julai, 2024 ambapo mtu yeyote anakaribishwa kupiga namba 0800112100 **kisha wakati huo huo au ndani ya dakika 20 atakuwa amepatiwa ufafanuzi au majibu au maelekezo ya hoja au maswali yake.**

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Kwa kumalizia, napenda kukushukuru tena kwa kukubali kuzindua zoezi hili la kitaifa. Ni matumaini ya Tume kuwa ushiriki wako katika kuzindua zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utasaidia kutoa hamasa kwa wananchi kujitokeza kushiriki katika zoezi hili.

Vilevile, Tume inaamini kuwa viongozi wa ngazi mbalimbali na wadau wengine wataendelea kuhamasisha wananchi katika maeneo yao ili kila mwananchi mwenye sifa ya kuandikishwa kuwa mpiga kura akaandikishwe na wale wanaohitaji kuboresha taarifa zao wakaboreshe.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA!!**

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA!!**